

Mimea ya mtama iliyokatwa baada ya majuma 4 toka kuvunwa hutoa nusu debe kwa kila ekari na wakati mwingine hakuna mavuno hata kidogo yanayopatikana.



Mavuno hafifu



### Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

#### Mtayarishaji:

Karanja, D. R.

#### Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

##### Mkurugenzi wa Kituo,

KARI Katumani

S.L.P. 340-90100 MACHAKOS

Simu: 044 20495, 20395/8


Nukulishi: 044 21122

Baruapepe: karikat@wananchi.com

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 14 /2008

**Shilingi 20 za Kenya**

## Kukata mtama na kuachilia kukua tena baada ya mavuno



## Utangulizi

### **Kuachilia mtama kukua tena baada ya kuvuna ni nini?**

Ni harakati za kukata mihimili ya mtama kiasi kidogo tu juu ya mchanga baada ya kuvuna ili inawiri na kukua tena.

Sampuli za mtama ulioboreshwa kama vile Gadam, Serena, Seredo na KARI mtama - I ina uwezo wa kukua tena baada ya kukatwa hivyo.

### **Kwa nini ikatwe ili kukua tena?**

- Mmea wa kukatwa hivyo hauhitaji mbegu msimu wa mvua chache.
- Mimea ya kukatwa na kukua upya hukomaa siku 20-30 mbele ikilinganishwa na mimea ya kawaida.
- Mvua inapopungua au kukosekana, mkulima aliyekata mimea yuaweza kupata kitu lakini wa kupanda upya hapati chochote.

### **Mmea wa mtama wa awali**

Mmea wa mtama wa mwanzo ni sharti ukuzwe kulingana na mapendekezo ya kilimo.

### **Hatua ya kwanza: Uvunaji mmea wa kwanza**

Vuna mimea ya kwanza kwa kukata sehemu iliyo komaa na kuacha mihimili inayosimama.



**Uvunaji mimea wa mwanzo**

### **Hatua ya pili: Ukataji wa shina**

Juma moja baada ya kuvuna, ikate tena mihimili ya mtama, kiwango wastani kutoka mchangani na itanawiri upya. Usisubiri hadi mimea ikauke.



**Ukataji tena wa mihimili**

### **Hatua ya tatu: Utunzaji wa shamba**

Baada ya kuvuna na kukata mihimili, ondoa majani ya mtama yaliyokatwa kutoka shambani kupunguza kuvamiwa na wadudu wanaotoboa mihimili.

Limia mimea mipya ya mtama na ufunike mchanga vizuri ili kuzuia kupotea kwa unyevu wa udongo.

### **Hatua ya nne: Kuvuna mtama wa pili**

Nafaka zinapokuwa tayari, vuna kama ulivyofanya kwanza.

Kuukata mtama juma moja baada ya kuvuna hutoa magunia manne zaidi kwa kila ekari ikilinganishwa na ukataji uliocheleweshwa au kutokatwa hata kidogo.



**Mavuno mazuri**